

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



“Nyamagana” Posta Road,
S.L.P. 2599,
MWANZA,
Barua Pepe: rbcmwanza@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

MWANZA – MEI 08, 2020

TAARIFA KWA UMMA

**UBADHIRIFU WA PEMBEJEO ZA KILIMO,
MHASIBU WA AM COS NA WAFANYABIASHARA 13
WASHIKILIWA NA TAKUKURU MWANZA.**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza, inamshikilia Mhasibu wa AMCOS ya MHEDI iliyopo wilayani Kishapu Mkoani Shinyanga, Wafanyabiashara 13 na Madalali 3 kwa makosa ya kujihusisha na vitendo vya rushwa kinyume na kifungu 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 pamoja kupatikana kwa mali iliyopatikana kwa njia isiyo halali kinyume na Kifungu cha 311 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu (Penal code) na marekebisho yake ya mwaka 2002.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Mwanza umebaini kuwa, Mhasibu huyo wa AMCOS ya MHEDI Bwana PAUL SYLIVESTER NKUBA maarufu kwa jina la NCHIMIKA amekuwa akifanya yafuatayo:

- (i) Akisafirisha na kuuza dawa za kilimo kutoka kwenye AMCOS ya MHEDI pamoja na AMCOS nyingine na kuzileta Mwanza kwa madalali na kwa wafanyabiashara wa maduka ya pembejeo za kilimo jijini Mwanza.
- (ii) Amekuwa akiwatumia madalali kusambaza dawa za kilimo kwenye maduka mbalimbali hapa jijini Mwanza. Dawa hizo za kilimo zilizokuwa zikifanyiwa ubadhirifu ni dawa zilizounuliwa na Serikali kupitia BODI YA PAMBA kwa lengo la kuwapatia wakulima wa pamba kupitia vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS).

Katika operesheni hii, TAKUKURU ilifanya upekuzi kwenye maduka ya pembejeo za kilimo kwa kushirikiana na BODI YA PAMBA baada ya kubaini kuwa dawa za bodi ya pamba zilizoletwa kwa lengo la kuwapatia wakulima kupitia AMCOS zilizopo kwenye maeneo yao zinauzwa kwenye maduka na wafanyabiashara.

Dawa hizo ambazo zimekutwa madukani zina thamani ya shilingi **Milioni 12,609,000/=** ambapo ni za aina zifuatazo:

- Banofos 100ml piece 286@6000;
- Banofos 250ml piece 62@15000,
- Banofos 500ml piece 48@30000/=,
- Ruruka 50gm piece 18@2000,
- Ruruka 100gm piece 372@4000;
- Ruruka 150gm piece 373@6000,

- Duduba piece 61@40000,
- Sosprid piece 189@5000,
- Mocron piece 5@20,000,
- Rapid attack piece 2@5000,
- Pump aina ya Matabi piece 8@180,000/=

Ndugu Waandishi wa Habari,

TAKUKURU mkoa wa Mwanza katika kuangalia namna bora zaidi ya kudhibiti vitendo vya rushwa katika eneo hili, ilifanya ufuatiliaji kwenye uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika vya Msingi – AMCOS. Katika ufuatiliaji huo tuliweza kubaini yafuatayo:

- Changamoto zinazowakabili wakulima wa pamba ni pembejeo kutowafikia kwa wakati
- Vilevile kuna ucheleweshwaji wa malipo ya wakulima mara baada ya kufanya mauzo.

Baada ya kubaini changamoto hizo TAKUKURU imefanya ufuatiliaji wa kutambua kwanini pembejeo za kilimo haziwafikii wakulima kwa wakati na ndipo ilipobaini kuwa baadhi ya viongozi wa AMCOS wasio waadilifu wamekuwa wakiyauza madawa hayo kwa wafanya biashara wa maduka ya dawa za kilimo.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika hatua nyingine, kwa muda mrefu TAKUKURU mkoa wa Mwanza imekuwa ikifuatilia madeni ya wakulima wa vyama vya msingi AMCOS na imeweza kuokoa fedha nyingi ambazo zimehujumiwa na baadhi ya viongozi wa AMCOS mbalimbali hapa Mkoani Mwanza.

Baadhi ya viongozi wa AMCOS wamekuwa wakizifanyia hujuma fedha za Serikali kwa kuandaa vocha za usambazaji wa pembejeo hewa za kilimo na kuidai fedha nyingi serikali, kukata kwa wakulima fedha za pembejeo za kilimo na kutoziwasilisha Serikalini na kufanya ubadhirifu wa pembejeo za kilimo kwa kuwauzia wafanyabishara badala ya wakulima.

Ifahamike kuwa zoezi hili ni endelevu na kwamba TAKUKURU haitovumilia kuona upotevu wa fedha za Serikali, hivyo uchunguzi wa tuhuma hizi bado unaendelea kwa kuwabaini wale wote wanaohusika na ubadhirifu huu na pindi uchunguzi utakapokamilika wahusika wote watafikishwa kwenye vyombo vya sheria kujibu tuhuma zinazowakabili.

TAKUKURU mkoa wa Mwanza inatoa onyo kwa viongozi wa AMCOS na wafanyabiashara wote kuacha tabia hiyo mara moja vinginevyo hatua kali zitachukuliwa kwa yoyote atakayebainika kuhusika na ubadhirifu wa pembejeo za kilimo.

Aidha tunawataka wakulima waendeleo kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU pindi wanapoona mambo hayaendi kwa mujibu utaratibu uliokusudiwa.

KWA PAMOJA TUTASHINDA VITA DHIDI YA RUSHWA

"Kwa taarifa za vitendo vya rushwa fika ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu nawe, tumia TAKUKURU APP, piga simu ya dharura namba 113 au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au Piga *113# fuata maelekezo" Huduma hii ni ya BURE.

IMETOLEWA NA:

SIGNED

EMMANUEL STENGA

MKUU WA TAKUKURU (M) MWANZA